MWONGOZO KWA SHULE ZA WATOTO WAKO



Kijitabu cha maelekezo cha Mzazi kwa Shule za Boise

Kuundwa na:
Shule ya Wilaya ya Boise, Programu za Shirikisho la Boise, Idaho

Fadhiliwa na:
Idara ya Elimu ya Jimbo la Idaho na Ofisi ya Makazi mapya ya Wakimbizi

SHUKRANI

Mwongozo kwa Shule za Watoto wako: Kijitabu cha maelekezo cha mzazi kimetokana na ushirikiano miongoni mwa mashirika mengi katika jimbo la Idaho. Watu wanaowajibika na maandalizi na uenezi wa kijitabu hiki cha maelekezo yanajumlisha:

Mike Stoy	Aliyekuwa Mshauri wa Wakimbizi Idara ya Elimu Jimbo la Idaho
Dkt. Ann Farris	Msimamizi wa Programu za Shirikisho Shule ya Wilaya ya Boise
Molly Jo de Fuentealba, M.Ed	Mshauri wa Programu za Shirikisho Shule ya Wilaya ya Boise

Shukrani maalum kwa Dkt. Edwin Silverman na Kituo cha Rasilimali cha Mafunzo ya Watu wazima cha Illinois kwa ukarimu wao wa kuturuhusu kuchukua vifaa kutoka kwenye *Mwongozo hadi katika Shule za Illinois za wazazi wa Wanafunzi wa LEP.*

Baadhi ya vifaa pia vilichukuliwa kutoka kwa wazazi kama Washiriki wa Elimu:
Mtaaala Husiani wa Wazazi Walio na upungufu wa Lugha na Laura Bercovitz na Catherine Porter, © the Adult Learning Resource Center.

KUHUSU KIJITABU HIKI CHA MAELEKEZO

Kwa Mzazi au Mlezi:

Karibu. Kijitabu hiki cha maelekezo kitakupatia maelezo muhimu kuhusu mfumo wa shule nchini Marekani na Idaho. Ikiwa wewe pamoja na familia yako ni wageni katika nchi hii au jimbo hili, pengine mna maswali yanayohusu shule. Maelezo kwenye kijitabu hiki cha maelekezo ni ya jumla. Tazama Sura ya X kwa ufafanuzi bainifu zaidi kuhusu wilaya ya watoto wako.

Wazazi na shule ni washiriki katika elimu ya watoto. Wote wanataka watoto kufanikiwa. Wakati wazazi na familia wanapojihusisha katika elimu, watoto wao wanafanya bora zaidi shuleni na kukua kwa ufanisi. Kwa kuelewa jinsi mfumo wa shule za Marekani unafanya kazi, unaweza kuwasaidia watoto wako kufaulu na kufanya bora zaidi kadri na uwezo wao.

JEDWALI LA MAUDHUI

MASWALI NA MAJIBU

I. MFUMO WA SHULE ZA MAREKANI

1. Ni vipi shule zimepangwa katika mji wangu?..... 6
2. Aina gani ya shule ambazo zipo Marekani.....……..... 7
3. Je, kunazo shule kwa wanafunzi ambao hawakamilishi elimu ya shule za upili?..... 9

II. KUJIANDIKISHA SHULENI

1. Nawezaje kuwaandikisha watoto wangu shuleni? Ni karatasi gani ambayo nahitaji?….. 10
2. Ni fomu zipi za matibabu na uchunguzi ambao watoto wangu wanahitaji kufanyiwa kabla waweze kuanza shule?.....……..... 10
3. Je, itakuwaje ikiwa watoto wangu walipewa chanjo hizi katika nchi yetu ya uraia au jimbo lingine?..... 11
4. Ni uchunguzi upi mwingine ambao watoto wangu wanahitaji?..... 11
5. Ni wapi tunaweza kwenda kwa uchunguzi wa kimwili?.....…. 11

III. KALENDA YA SHULE NA SIKU YA SHULE

1. Ni muda upi watoto wangu watamaliza shuleni kila siku?..... 12
2. Je, kunazo siku za likizo au siku maalum ambapo watoto hawaendi shuleni?..... 12

IV. KUENDA SHULENI

1. Je, ni jinsi gani watoto wangu watakavyoenda na kurudi kutoka shuleni?..... 14

V. UTARATIBU WA SHULE

1. Nitafanya nini ikiwa mtoto wangu anagonjeka?..... 15
2. Je, itakuwaje ikiwa mtoto wangu lazima atumie dawa shuleni?..... 15
3. Nitapigia nani simu ikiwa nina maswali kuhusu afya ya mtoto wangu?..... ..... ….... 16
4. Shule itanifikia vipi ikiwa mtoto wangu ataugua akiwa shuleni au kupata ajali?.... 17
5. Je, ikiwa mtoto wangu lazima achelewe au kukosa kufika shuleni, natakiwa kufanya nini?.… .....…….. 18
6. Naweza kuitembelea shule ye mtoto wangu?.....…… 19
7. Nahitaji kulipia chochote shuleni?.....……..... 19
8. Ni nani nitauliza kuhusu utaratibu wa shule ikiwa nina swali?.....…… … 20

VI. WATU WANAOFANYA KAZI SHULENI

1. Ni watu wapi ambao wanafanya kazi katika afisi za wilaya za shule na kwenye shule? 21

2. Ni watu wapi ambao wanafanya kazi katika afisi za wilaya za shule na kwenye shule? 23

VII. PROGRAMU ZA KUFUNDISHA

1. Je, shule itafanya nini ili kusaidia, ikiwa watoto wangu hawazungumzi Kiingereza vizuri?.. 24
2. Ni masomo yapi ambayo watoto wangu wanajifunza katika shule ya msingi?..... 24
3. Ni masomo yapi ambayo watoto wangu wanajifunza katika shule ya kati au shule ya upili ya ngazi ya chini?…..... 24
4. Ni masomo yapi ambayo watoto wangu wanajifunza katika shule ya upili?..... 25
5. Ikiwa mtoto wangu ana matatizo ya kusoma au mahitaji maalum, je, shule itafanya nini ili kusaidia?..... 26
6. Je, kunazo program maalum ikiwa mtoto wangu ana kipaji au uwezo maalum?..... ….. 26

VIII. JUKUMU LA WAZAZI KATIKA ELIMU NA MASOMO YA WATOTO WAO

1. Nitajifunza vipi kuhusu shule ya mtoto wangu? Je, mtoto wangu ni mwanafunzi mzuri?..... 27
2. Nitajua vipi jinsi watoto wangu wanafanya shuleni?.....……..... 28
3. Nitasaidiaje kufanya uamuzi kuhusu shule?.....…..……... 29
4. Ni shughuli zipi maalum ambazo naweza kuhudhuria katika shuleni ya watoto?..... 30
5. Ni nia zipi ambazo naweza kujitolea katika shule ya watoto wangu?..... 31
6. Nitafanya nini nyumbani ili kusaidia masomo ya watoto wangu?.....……... 32
7. Nitafanya nini ili kusaidia watoto wangu kupanga maisha yao baada ya shule ya upili? 37

IX. ELIMU YA WATU WAZIMA

1. Nitaenda wapi kujifunza Kiingereza au kuhudhuria masomo mengine?.....…….. 36

X. SHULE ZA BOISE

1. Nitamwandikisha vipi mtoto wangu?.....…. 39
2. Ni shule gani ambayo watoto wangu watajiunga nayo?.....…. 39
3. Ni program zipi ambazo Boise inazo kwa wanafunzi wa shule ya ngazi ya chini nay a upili? 39
4. Watoto wangu watafika vipi shuleni?..... 40
5. Nitalipia nini shuleni?.....…….. 41
6. Je, mtoto wangu anaweza kuchelewa au kukosa kwenda shuleni?.....…. 43
7. Je, mtoto wangu anaweza kuondoka shuleni mchana?..... …….. 43
8. Ni nini kinachokataliwa shuleni?.....…….. 44
9. Ni nini kitafanyika kwa wanafunzi ambao huleta silaha shuleni?..... …… 44
10. Naweza kupata wapi maelezo ya ziada kuhusu Shule ya Wilaya ya Boise?.. . … 44
11. Nitapata wapi maelezo kuhusu Programu za Lugha ya Kiingereza kwa Mwanafunzi?.... 45

I. MFUMO WA SHULE YA MAREKANI MMMM

Katika Idaho, watoto wote waliyo na umri wa miaka 7 hadi 16 lazima waende shuleni. Mwaka wa shule huanza mwisho wa Agosti au mapema Septemba na hukamilika mwezi wa Juni. Kunayo karibu miezi mitatu ya likizo ya majira ya joto mnamo Juni, Julai na Agosti.



Katika nchi ya Marekani kunazo shule za umma na binafsi. Shule za umma hazilipishi na shule za binafsi hutoza karo inayojulikana kama masomo. Pesa ambazo zinalipwa kwenye shule za umma hutoka kwenye ushuru wa rasilimali katika jumuiya yako. Ikiwa unamiliki nyumba yako, sehemu ya ushuru wa rasilimali yako husaidia kulipia shule za umma. Mmiliki wa jengo hutumia sehemu ya kodi yako kwa ushuru huu. Serikali pia husaidia kulipa shule za umma na pesa ningine.

1. Shule zimepangwa vipi katika mji wangu?

Wilaya za Sule na Bodi za Shule

Katika nchi ya Marekani, shule za umma zimegawanywa katika wilaya. Baadhi ya wilaya za shule zinajumlisha tu jiji au mji mmoja, lakini nyingine zinajumlisha zaidi ya jiji au mji mmoja.

Kila wilaya ya shule ina bodi ya shule. Wanachama wa bodi ya shule huishi katika wilaya zao za shule. Bodi ya shule hufanya uamuzi kuhusu shule katika wilaya. Kwa mfano, bodi ya shule huamua ikiwa wilaya inahitaji kujenga shule mpya. Bodi ya shule pia huchagua msimamiaji. Msimamiaji ni mkurugenzi wa wilaya ya shule.

2. Ni aina zipi za shule ambazo zipo Marekani?

Kuna aina nyingi za shule nchini Marekani.

Shule ya maandalizi (miaka 3 au 4): Badhi ya watoto huenda katika shule za maandalizi, watoto hucheza na watoto wengine na kujifunza mapema hisabati na mbinu za kusoma. Kwa kawaida watoto huhudhuria saa chache kwa siku kwa siku 2, 3 au 5 kwa wiki. Sio kila shule ina shule ya maandalizi. Baadhi ya shule za maandalizi hazilipishi na nyingine hutoza karo ya masomo.

Chekechea (umri 5): Ikiwa watoto wana umri wa miaka 5 mnamo au kabla ya Septemba 1, wanaweza kuenda chekekea. Watoto sio lazima waende chekechea, lakini watoto wengi huenda. Wanaenda chekechea kutoka Jumatatu hadi Ijumaa. Masomo mengi ya chekechea ni ya siku nusu, na mengine ni ya siku nzima.

Gredi 1 – 9 (Msingi/Kati/Shule ya Upili ya Ngazi ya chini): Miaka ya shule nchini Marekani inaitwa "gredi". Watoto wanahudhuria shule saa 5-1/2 - 7 kila siku kutoka Jumatatu hadi Ijumaa. Watoto wachanga kwa kawaida hukaa kwenye darasa moja na wana mwalimu mmoja kwa kipindi chote cha mwaka shuleni. Wanafunzi wakubwa kwa kawaida huwa na madarasa 6 hadi 8 tofauti wakati wa siku. Huenda wakabadilisha madarasa tofauti na huenda wakawa na waalimu tofauti kwa kila somo. Shule za watoto katika gredi 5 au 6 hadi 8 zinaitwa Shule za Kati au Shule za Upili za Ngazi ya chini.

Gredi 10 – 12 (Shule ya Upili): Watoto kwa kawaida hujiunga na shule ya upili wakiwa na umri wa miaka 15 na waliyohitimu wakiwa na umri wa miaka 18. Wanafunzi wa shule ya upili hubadilisha madarasa na wanakuwa na waalimu tofauti wakati wa siku. Wanapata alama za kila somo, ambazo zinahitajika kwa kuhitimu. Shule za upili huwaandaa wanafunzi kwa kazi au kwa mafunzo katika chuo cha elimu ya juu katika jumuiya au chuo kikuu.

Mipango za Kablya na Baada ya Shule: Baadhi ya shule zina program za uangalizi kwa mtoto kabla ya shule. Katika shule hizi, wazazi wanaweza kuwaleta watoto wao shuleni kabla ya shule kuanza. Baadhi ya shule pia zina programu ya watoto bada ya shule. Katika shule hizi, watoto wanaweza kujiandikisha kwa programu ya baada ya shule ya muziki, michezo, msaada wa zoezi la nyumbani au shughuli nyingine. Baadhi ya shule hutoza karo kwa programu hizi.

Lazima uwaandikishe watoto wako katika programu maalum na upeane kibali chjako kilicho kwenye maandishi kabla watoto wako waweze kuja mapema au kuchelewa baada ya shule.

Shule ya Majira ya joto: Shule nyingi za msingi na za upili hutoa mafunzo ya majira ya joto. Baadhi ya mafunzo katika majira ya joto ni ya wanafunzi ambao wanahitaji msaada wa ziada shuleni. Baadhi ya mafunzo ni ya shughuli au mada maalum, kama vile mafunzo ya kompyuta au mafunzo ya maudhui ya Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza. Kunaweza kuwa na karo ya shule ya majira ya joto.

Baada ya Shule ya Upili: Wanafunzi wanaohitimu kutoka shule ya upili wanaweza kuchagua kwenda kufanya kazi au kujiunga na jeshi. Wanaweza pia kutaka kuendelea kusoma katika shule za kiufundi, vyuo vya elimu ya juu katika jamuiya, au miaka 4 katika vyuo vya elimu ya juu na vyuo vikuu nchini Marekani. Vyuo vikuu na vyuo vya elimu ya juu vya binafsi na umma huenda vikawa na gharama ya juu zaidi. Wanafunzi wanaweza kuomba ufadhili na mikopo ili kuwasaidia kugharamia elimu yao. Watu wengine wachanga wanajiunga na jeshi ili kupata elimu ya bila malipo.



Kuna vyuo vingi vya elimu ya juu ya miaka 4 na vyuo vikuu vya binafsi na umma nchini Marekani. Vyuo vikuu vya binafsi na umma na vyuo vya elimu ya juu ya miaka 4 huenda vikawa vya gharama ya juu. Wanafunzi wanaweza kuomba ufadhili na mikopo ili kuwasaidia kugharamia elimu yao. Watu wengine wachanga wanajiunga na jeshi ili kupata elimu ya bila malipo.

Vyuo vya elimu ya juu vya jumuiya ni shule za umma za miaka 2 zinazofadhiliwa na ushuru wa rasilimali na serikali. Vina gharama chache kuliko vyuo vya binafsi au umma. Baada ya kuhudhuria chuo cha elimu ya juu cha jumuiya, wanafunzi wanaweza kupokea digri ya Mshirika wa Sanaa au uhamisho katika chuo kikuu kwa kipindi cha miaka 4 ili kuendelea na masomo yao.

Maelezo ya Ziada

3. Je, kunazo shule kwa wanafunzi ambao hawakamilishi elimu za upili?

Lazima watoto wahudhurie gredi 1-12 ili kuhitimu kutoka kwa shule ya upili. Ni muhimu kuhitimu kutoka shule ya upili. Vyuo vingi na waajiri huhitaji stashahada ya shule ya upili. Lakini wanafunzi wengine huondoka kwenye shule ya upili kabla ya kuhitimu. Wanaacha shule. Kunazo programu tofauti za wanafunzi hawa:

Masomo ya jioni: Baadhi ya shule za upili zina masomo ya jioni kwa wanafunzi walioacha shule.

Shule Mbadala ya Upili: Baadhi ya wilaya zina shule mbadala za upili. Hizi kwa kawaida ni shule ndogo kwenye jingo tofauti kuliko shule ya kila mara ya upili.

Masomo ya GED: Kuna masomo ya siku na ya jioni ili kuwasaidia watu wazima kupita majaribio ya Maendeleo ya Elimu ya Kawaida (GED). Watu wazima wanaweza kutumia GED kama stashahada ya shule ya upili. Vyuo vikuu vingi na waajiri wanakubali GED. Matawi ya ndani ya maktaba ya umma kwa kawaida yana maelezo kuhusu masomo ya GED.

Maelezo ya Ziada

II. KUJIANDIKISHA SHULENI

1. Nawezaje kuwaandikisha watoto wangu shuleni? Ni karatasi gani ambayo nahitaji?

Makaratasi ambayo unaweza kuhitaji kwa kujiandikisha:

- Thibitisho ya tarehe ya kuzaliwa ikiwa inapatikana (cheti cha kuzaliwa cha mtoto, I-94, au paspoti ya mtoto)
- Nambari ya Usalama wa Jamii ikiwa inapatikana
- Nyaraka za Afra: Rekodi za Chanjo
- Thibitisho ya anwani: (Proof of address: (bili ya gharama, kukodisha nyumba, leseni halali ya dereva wa Idaho, hati tambulishi (taarifa ya kuapishwa) ya makazi
- Nakala kutoka shule ya awali ikiwa zinapatikana. Kwa mfano, wazazi wanaweza kuwa na rekodi za shule kutoka shule nyingine za Marekani au kutoka kwa shule za nchi zao asili.

Uliza shule orodha ya makaratasi ya kuleta ya kujiandikisha.

2. Ni fomu zipi za matibabu na uchunguzi ambao watoto wangu wanahitaji kufanyiwa kabla waweze kuanza shule?

Wakati watoto wanaingia shuleni, lazima wawe na chanjo za sasa. Ikiwa chanjo hazijasasishwa, hawataruhusiwa kuhudhuria mafunzo wakati shule zinapoanza..

Chanjo: Wanafunzi wote lazima wapewe chanjo (kutibiwa) dhidi ya magonjwa bainifu. Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na mfanyikazi wa kesi yako, mfadhili, au nesi wa shule.

Uchunguzi wa kimwili: Kabla ya kujiandikisha kwenye P.E. au mchezo katika shule ya kati au ya upili, mwanafunzi pia lazima afanyiwe uchunguzi wa kimwili. Daktari atajaza fomu ya matibabu. Utahitajika kurudisha fomu iliyojazwa kikamilifu shuleni.

3. Je, itakuwaje ikiwa watoto wangu walipewa chanjo hizi katika nchi yetu ya uraia au jimbo linguine?

Ikiwa mtoto alipewa baadhi ya chanjo hizi katika nchi nyingine au jimbo, wazazi wanafaa kuonyesha daktari rekodi ya matibabu wakati wa uchunguzi wa kimwili wa mtoto. Daktari atapeana rekodi ya chanjo ya Marekani. Ikiwa hakuna rekodi ya matibabu ya chanjo, lazima mtoto apewe chanjo tena.

4. Ni uchunguzi upi mwingine ambao watoto wangu wanahitaji?

Katika shule nyingi za msingi, watoto wanapokea uchunguzi wa matatizo ya kuona (macho) au kuskia (maskio). Watoto ambao wana valia miwani hawapokeai uchunguzi wa kuona. Ikiwa uchunguzi unaonyesha matatizo ya kuona au kusikia kwa mtoto, shule inamtumia mzazi wa mtoto babua. Ikiwa utapokea babua kutoka shuleni, unafaa kumpeleka mtoto wako kwa daktari au kwenye kliniki kwa uchunguzi kamili.

5. Ni wapi tunaweza kwenda kwa uchunguzi wa kimwili?

Watoto wanaweza kupata uchunguzi wa kimwili na chanjo katika afisi ya daktari au kliniki. Shule zote zina maelezo kuhusu uchunguzi na chanjo ya bila malipo au gharama ya chini.

Maelezo ya Ziada

III. KALENDA YA SHULE NA SIKU YA SHULE

1. Ni muda upi watoto wangu watamaliza shuleni kila siku?

Shule nyingi huanza mwishoni mwa Agosti au mapema Septemba na kumalizika wiki ya kwanza au ya pili Juni. Siku ya shule kwa kawaida ni karibu saa 5-1/2 – 7 kwa urefu. Kwa kawaida wanafunzi hula chakula cha mchana shuleni. Watoto wengine huja na chakula shuleni. Wanafunzi pia wanaweza kununua chakula cha mchana shuleni.

2. Je, kunazo siku za likizo au siku maalum ambapo watoto hawaendi shuleni?

Siku kuu ya wafanya kazi.....	Septemba 1, Jumatatu
Kurudisha shukrani..... ...	Novemba 4, Alahamisi
Krismasi.....	Disemba 25
Miaka mipya.....	January 1
Siku kuu ya Martin Luther King	Januari 3, Jumatatu
Siku kuu ya Rais.....	Februari 3, Jumatatu
Siku kuu ya Kumbukumbu.....	Mei 4, Jumatatu

Shule zinafungwa kwa siku nyingine vile vile. Shule huweka baadhi ya likizo zake. Kuna mikutano maalum ya waalimu katika Siku za Taasisi. Wakati mwingine hakuna shule katika siku za huduma ya ndani, na wakati mwingine watoto huenda nyumbani mapema. Wakati watoto wanaenda nyumbani mapema, inajulikana kama kutolewa mapema. Kalenda ya shule huorodhesha wakati watoto wanakaa nyumbani siku za huduma ya ndani, siku kuu, likizo, au kutolewa mapema. Ikiwa mtoto wako anahitaji kukaa nyumbani siku ya dini wakati ambapo shule haijafungwa, piga simu shuleni ili kuripoti kukosa kwa mtoto wako kuhudhuria shule.

Kufunga Shule: Wakati mwingine shule hufunga wakati hali ya anga ni mbovu. Kwa mfano, ikiwa kuna theluji nyingi nje au kuna kimbunga, shule inaweza kufunga. Unaweza kusikiliza kwenye redio kutazama taarifa kwenye runinga asubuhi kuona ikiwa shule za watoto wako zimefungwa.

MADOKEZO MUHIMU

Uliza kalenda ya shule wakati unamwandikisha mtoto wako.

Maelezo ya Ziada

IV. KUENDA SHULE

1. Je, ni jinsi gani watoto watakavyoenda na kurudi kutoka shuleni?

Watoto ambao wanaishi karibu na shule kwa kawaida wanatembea wa kienda shuleni. Watoto ambao wanaishi mbali na shule kwa kawaida huletwa na basi la shule au huchukua usafiri wa umma. Mabasi ya shule ni ya bila malipo. Ikiwa mtoto wako ataabiri basi la shule, unahitaji kujua:

- nambari ya basi la shule
- mahali mtoto wako anaabiria basi
- saa ambayo mtoto wako anaabiri basi
- mahali mtoto wako anashuka kutoka kwenye basi
- saa ambayo mtoto wako anashuka kutoka kwenye basi



Nambari ya Basi	
Mahali pa Kuchukuliwa	
Saa ya Kuchukuliwa	
Nambari ya Basi	
Mahali pa Kushukishwa	
Saa ya Kushukishwa	

V. UTARATIBU WA SHULE

1. Nitafanya nini ikiwa mtoto wangu anagonjeka?

Ikiwa watoto ni wagonjwa, wanafaa kukaa nyumbani. Wakati mwingine mzazi anamtuma mtoto mgonjwa shuleni kwa sababu wanafaa kwenda kazini na hawawezi kukaa nyumbani na mtoto. Lakini mtoto mgonjwa kila mara huwafanya watoto wengine kugonjeka. Shule nyingi hazitaki wazazi kutuma mtoto wao shuleni ikiwa:



- mtoto ana homa ya nyuzi 100° F (37.7° C) au juu zaidi
- mtoto alitapika usiku kala au asubuhi kabla ya shule
- mtoto anakohoa zaidi
- mtoto ana upele au vidonda mwilini
- mtoto ana chawa (Wazazi lazima waoshe nwele ya mtoto na shampuu maalum na kutoa mayai kwenye nywele. Baada ya haya, mtoto anaweza kurudi tena shuleni.)
- mtoto ana tetekuwanga (Mtoto lazima akae nyumbani kwa siku saa baada ya kuanza kwa tetekuwanga.)
- mtoto ana maumivu ya koo (Mtoto anaweza kurudi shuleni baada ya kutumia viua vijasumu kwa saa 24-48.)
- mtoto ana homa nyekundu (Mtoto anaweza kurudi shuleni baada ya kutumia viua vijasumu kwa saa 24-48.)
- mtoto ana kiwambo ute cha jicho (pinkeye)

Shule kwa kawaida hutuma barua kwa wazazi ikiwa mwanafunzi kwenye darasa la mtoto wao ana ugonjwa wa kuambukiza kama vile tetekuwanga, maumivu ya koo, homa nyekundu, homa, au chawa. Barua hii inakueleza kile cha kuangali kwa hivyo utajua ikiwa mtoto wako ameambukizwa ugonjwa.

2. Je, itakuwaje ikiwa mtoto wangu lazima atumie dawa shuleni?

Wazazi hawafai kuwatuma watoto wao shuleni na dawa labda tu kama ni muhimu zaidi. Watoto hawaruhusiwi kutumia dawa wenyewe shuleni. Ikiwa ni muhimu mtoto mtoto kutumia dawa shuleni, wazazi wanafaa kuandika maelezo ya kufafanua hali na kupeana kwa katibu wa shule. Mtoto lazima alete dawa afisini. Baadhi ya shule zinaweza kuhitaji maelezo ya daktari. Wazazi wanafaaa kutuma dawa shuleni ikiwa kwenye chupa asili ya famasia, sio kwenye mkoba au bahasha. Chupa lazima iwe na lebo ya:

- jina la mtoto
- jina la daktari
- jina la dawa
- kiasi na wakati wa kupeana dawa

Mtoto alzima aje afisini kuchukua dawa.

3. Nitapigia nani simu ikiwa nina maswali kuhusu afya ya mtoto wangu?

Ikiwa unalo swali kuhusu afya ya mtoto wako shuleni, pigia simu katibu wa shule au mshauri. Ikiwa unaripoti kukosa kuhudhuria, pigia katibu wa shule simu.

Maelezo ya Ziada

4. Shule itanifikia vipi ikiwa mtoto wangu ataugua akiwa shuleni au kupata ajali?

Ikiwa mtoto wako ataugua au kupata ajali shuleni, shule itakupigia simu au mtu aliye kwenye Kadi za Dharura.

Maelezo ya Kadi ya Dharura: Shule itakupatia fomu hii wakati unawaandikisha watoto wako shuleni. Kwenye Kadi ya Dharua, andika jina na nambari ya simu ya mtu wa kupigia simu ikiwa mtoto ni mgonjwa au amepata ajali shuleni. Ni muhimu kujaza kadi ya dharura ya kila mtoto na kuituma shuleni.

Ni muhimu kuandika:

- nambari ya simu ya mahali ulipo wakati wa mchana
- jina na nambari ya simu ya mtu wa jamii au rafiki wa karibu ambaye anaelewa Kiingereza
- jina na nambari ya simu ya daktari au kliniki ya mtoto wako
- mahitaji yoyote muhimu ya afya ambayo mtoto wako anayo

Nambari Yako ya Simu ya Mchana	☎
Jina la Rafiki & Simu	☎
Jina la Daktari/Kliniki & Simu	☎
Mahitaji maalum ya mtoto wangu:	

Ikiwa maelezo haya yatabadilika wakati wowote, wasiliana na jaza Kadi mpya ya Dharura.

Kuhama: Ikiwa utahamia kwenye ghorofa au nyumba nyingine, unafaa kuwasiliana na shule na kuwapatia anwani mpya na nambari ya simu. Pia unafaa kujaza Kadi mpya ya Dharura.

Je, ikiwa mtoto wangu lazima achelewe au kukosa kufika shuleni, natakiwa kufanya nini?

Kuchelewa Shuleni: Watoto hawafai kuchelewa shuleni. Watoto wanafaa kukuja kwa saa inayohitajika. Ikiwa watoto watachelewa, mwalimu atatia alama kama wamechelewa au tadi. Unafaa kupiga simu shuleni asubuhi ikiwa mtoto wako atachelewa. Au unaweza kutuma mtoto wako na akienda shuleni.

Kukosa kufika Shuleni: Wakati mtoto wako hawezi kukuja shuleni, piga simu shuleni kila siku asubuhi kabla shule kuanza. Baadhi ya shule zina mashine ya kupokea. Wazazi wanaweza kuacha ujumbe kwenye mashine ya shule ya kujibu.

Wakati unapiga simu shuleni, unafaa kupeana maelezo yafuatayo:

- jina la mtoto wako
- gredi ya mtoto wako na mwalimu
- kwa nini mtoto wako atakosa kwenda shuleni
- jina lako na nambari ya simu

Wakati mwingine wazazi huwachukua watoto wao shuleni wakati wa mchana kabla muda wa shule kuisha. Huenda wanataka kuwapeleka watoto wao kwa daktari au daktari wa meno wakati wa mcvhana. Ikiwa unataka kuwachukua watoto wako kutoka shuleni, lazima umwandikie mwalimu maelezo. Mtoto wako anapaswa kumpelekea mwalimu maelezo asubuhi. Maelezo yanastahili kuwa na sababu zifuatazo:

- kwa nini unamchukua mtoto wako kutoka shuleni
- saa ambayo utamchukua mtoto wako kutoka shuleni
- jina la mtu anayemchukua mtoto wako ikiwa yeye sio mzazi au mlezi

Wakati unaenda shuleni kumchukua mtoto wako, nenda afisini na umuulizie mtoto wako. Shule itakutaka kutie sahihi kwenye karatasi ili mtoto wako aweze kuondoka.

Likizo za Fimilia: wazazi hawapaswi kuwapeleka watoto wao kwenye likizo wakati wa shule. Wazazi wanafaa kuchukua likizo za familia wakati wa likizo za shule. Ikiwa ni lazima uchukue likizo yako wakati wa shule, unapaswa kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako kabla ya kuenda.

Kazi ya Kujitengenezea: Watoto ambao wanakosa kwenda shuleni lazima wafanye mazoezi ya shuleni na mazoezi ya nyumbani ambayo wamekosa. Ikiwa

mtoto anakosa kwenda shuleni kwa siku 2, shule nyingi huwataka wazazi kupiga simu shuleni ili kupata zoezi la kujitengenezea. Wewe au rafiki ya mtoto wako anaweza kwenda katika darasa la mtoto ili kupata zoezi la kujitengenezea.

5. Naweza kutembelea shule ya mtoto wangu?

Kutembelea shule: Wazazi wanakaribishwa kutembelea shule za watoto wao. Wakati unapotembelea shule, lazima uende afisini ili upewe idhini ya mgeni. Unaweza kutembelea darasa la mtoto wako, lakini huwezi kuzungumza na mwalimu kuhusu mtoto wako wakati wa masomo. Ikiwa wazazi wanataka kuzungumza na mwalimu, lazima waweke miadi mapema.

6. Naweza kulipia chochote shuleni?

Kuna malipo ya baadhi ya shughuli au vifaa vya shule:

Malipo ya vitabu: Kuna malipo ya vitabu kwa baadhi ya viada. Ikiwa malipo ya kitabu ni ya juu zaidi kulipwa na familia, wazazi wanaweza kuzungumzo na shule kuhusu malipo yaliyopunguzwa au kuondolewa. Mtoto wako lazima avitunze vizuri vitabu hivyo. Mnamo mwishoni mwa mwaka wa shule, mtoto wako atahitajika kurudisha vitabu vyote shuleni.

Shughuli za ziada: wakati mwingine malipo ya shughuli za ziada kama vile michezo, vipindi vya muziki, au academia au vilabu vya mapatano. Nyingi kati ya shughuli hizi zinafanyika baada au kabla ya shule kuanza.

Safari za uga: Wakati mwingine wanafunzi wanaenda katika safari za ugani katika makumbusho, zoos, na mahali kwingine. Wazazi lazima watie sahihi kwenye fomu ya idhini kabla ya mtoto kuweza kwenda katika safari ya ugani. Wakati mwingine kuna malipo kiasi ya kusaidia kulipia safari ya ugani. Wakati mwingine wazazi wanapewa nafasi ya kujitolea kwenda katika safari ya ugani ili kumsadia mwalimu kuwaangalia watoto safarini.

Chakula cha mchana: Ikiwa watoto hawaji na chakula chao cha mchana shuleni, Shule nyingi zina programu za bila malipo au gharama ya chini ya chakula cha mchana kwa wazazi ambao hawawezi kulipa. Wazazi wanapaswa kujaza fomu kuhusu mapato ya familia ili kuona ikiwa watoto wao wanaweza kupokea chakula cha mchana cha bila malipo au gharama ya chini.

7. Ni nani nitauliza kuhusu utaratibu wa shule ikiwa nina swali?

Unaweza kumpigia mwalimu wa mtoto wako ikiwa una swali kuhusu utaratibu wa shule.



Maelezo ya Ziada

VI. WATU WANAOFANYA KAZI SHULENI

1. Ni watu wapi ambao wanafanya kazi katika afisi ya shule na kwenye shule?

Watumishi wa shule ni watu ambao wanafanya kazi shuleni. Kuna aina tatu ya watumishi wa shule: wasimamizi, waalimu, na wasaidizi wa shule.

Watawala hawafundishi wanafunzi. Wanasimamia shule na programu. Kuna aina tofauti ya watawala:

Wasimamiaji:	Msimamiaji ni mtawala wa wilaya ya shule.
Mwalimu mkuu:	Kila shule wilayani ina mwalimu mkuu ambaye ni mtawala wa shule.
Naibu ya mwalimu mkuu::	Wakati mwingine shule zina naibu wa kumsaidia waalimu wakuu.
Afisi ya Kati:	Utawala wa wilaya ambao unafanya uamuzi mpana wilayani.

Waalimu wanawafundisha watoto shuleni. Kuna aina nyingi tofauti ya waalimu:

- *Mwalimu wa darasani:* Katika chekechea kupitia greidi ya 5 au 6, wanafunzi kwa kawaida hukaa na mwalimu wao wa darasani wakati wa siku ya shule. Mwalimu wa darasa kwa kawaida hufunza masomo mengi kama vile kusoma, hisabati, na sayansi.

- *Mwalimu wa Chumba cha nyumbani/Timu:* Katika shule ya kati, ngazi ya chini na upili, wanafunzi wana mwalimu wa chumba cha nyumbani. Wakati mwingine wanashiriki kwenye shughuli za kikundi zinazoitwa ushauri. Wakati wa chumba cha nyumbani, wanafunzi wanaskiza matangazo na kupata habari kuhusu siku ya shule.

- *Mwanafunzi wa Mwanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (ELL):* Mwalimu wa ELL hufunza Kiingereza wanafunzi ambao wanahitaji maagizo ya kusoma, kuandika, na kuzungumza kiingereza.

- *Mwalimu Maalum wa Elimu:* Mwalimu maalum wa elimu hufunza wanafunzi walio na mahitaji maalum. Wanafunzi hawa lazima wahitimu kupitia kwa mkutano unaoitwa "IEP" (Mpango wa Elimu ya Kibinafsi).

- *Mwalimu aliye na Kipawa:* Mwalimu aliye na kipawa hufunza madarasa ya wanafunzi ambao wanapata alama za juu kwenye jaribio na/au wanafunzi waliyo na talanta haba.

- *Mwalimu wa Muziki:* Mwalimu wa muziki anafunza dansi, kuimba na jinsi ya kucheza ala za muziki.

- *Mwalimu wa Sanaa:* Mwalimu wa sanaa hufunza kupaka rangi, kuchora, The art teacher teaches painting, drawing, kufinyanga udongo, na zana nyingine.

- *Mwalimu wa koboresha viungo/Mwalimu wa Elimu ya Kimwili (PE)* Mwalimu wa koboresha viungo au wa elimu ya kimwili hufunza elimu ya kimwili kama vile michezo na mazoezi.

- *Mkutubi:* Mkutubi huwasomea wanafunzi na kuwafunza kuhusu maktaba na huwasaidia wanafunzi kuazima vitabu kutoka maktabani.

- *Mwalimu wa Hotuba:* Mwalimu wa hotuba huwasaidia wanafunzi ambao wana ugumu wa kutamka na kuongea. Wanafunzi hawa lazima wahitimu kupitia kwa mkutano wa "IEP" (Mpango wa Elimu ya Binafsi).

Wafanyakazi wa Msaada wanasaidia watawala na waalimu kufanya kazi yao. Baadhi ya wafanyakazi wa msaada ni:



- *Katibu wa Shule:* Katibu hupokea simu, aina ya barua na maelezo, huwaamkua wageni wa shule, na husaidia mwalimu mkuu.

- *Nesi ya Shule:* Nesi wa shule au katibu humuhudumia mtoto mgonjwa shuleni.

- *Mfanyakazi wa Jamii/Mshauri:* Mfanyakazi wa jamii au mshauri husaidia wanafunzi walio na matatizo wanayokumbana nayo shuleni au nyumbani. Mfanyakazi wa jamii anaweza kufanya kazi na mtoto, mzazi au familia nzima. Katika shule ya upili, mshauri huwasaidia wanafunzi kuchagua masomo na kuwapatia maelezo kuhusu vyuo vya elimu ya juu au kazi.

2. Naweza kuongea na nani shuleni kuhusu mtoto wangu?

Katika shule za msingi, zungumza kwanza na mwalimu wa darasa au ELL ya mtoto wako. Atakusaidia au kukuambia nani anaweza kukusaidia.

Katika shule ya kati, ngazi ya chini au upili, unaweza kwanza kumpigia mwalimu wa chumba cha nyumbani au ELL.

Mwanzo mwa mwaka wa shule, jaza maelezo kwenye jedwali hili kuhusu watoto wako:



Jina la Mtoto	Jina la Shule	Nambari ya Simu ya Shule	Gredi	Jina la Mwa
		☎		
		☎		
		☎		

Maelezo ya Ziada

VII. PROGRAMU ZA KUFUNDISHA

1. Je, shule itafanya nini ili kusaidia, ikiwa watoto wangu hawazungumzi Kiingereza vizuri?

Wanafunzi ambao wana ugumu wa kuzungumza au kuandika Kiingereza wanaweza kuchukua Kiingereza kama somo la pili la lugha ya Kiingereza (ESL) shuleni. Masomo ya ESL hufunza wanafunzi kuzungumza, kusoma na kuandika Kiingereza. Pia wanafunza Kiingereza kupitia kwa maudhui kama vile historian a sayansi.

Wakati wanafunzi wanajiandikisha shuleni mara ya kwanza, wanafanya jaribio la Kiingereza. Jaribio huisaidia shule kuwaweka wanafunzi katika madarasa yanayohitajika. Wanafunzi walio kwenye programu za ELL hufanya jaribio la Kiingereza kila mwaka. Wanafunzi hupata mafunzo yao ya ELL hadi ujuzi wao wa Kiingereza uhimarike.

2. Ni masomo yapi ambayo watoto wangu wanajifunza katika shule ya msingi?

Watoto hujifunza mtaala wa shule ya wilaya. Katika shule ya msingi, watoto hujifunza masomo mengi tofauti:

- kusoma, sanaa za lugha, na hisabati (kila siku)
- afya, sayansi, mafunzo ya jamii (mara 2 hadi 5 kwa wiki)
- sanaa, elimu ya kimwili, maktaba, muziki (mara 1 au 2 kwa wiki)

3. Ni masomo yapi ambayo watoto wangu wanajifunza katika shule ya kati au shule ya upili ya ngazi ya chini?

Katika shule ya kati au shule ya ngazi ya chini, kwa kawaida watoto hubadilisha madarasa ya masomo. Kwa kawaida wanakuwa na waalimu tofauti wakati wa siku. Wanakaa kwenye jengo wakati wa mchana na hawana mapumziko. Masomo ambayo wanasoma huenda yakawa:

- Kusoma & Sanaa ya Lugha
- Elimu ya Kimwili & Afya
- Sayansi
- Masomo ya Jamii
- Muziki
- Hisabati
- Kompyuta
- Sanaa
- Lugha za Kigeni (kwa mfano, Kihispania &Kifaransa)

4. Ni masomo yapi ambayo watoto wangu wanajifunza katika shule ya upili?

Wanafunzi wa shule ya upil wanachukua kozi zinazohitajika na za hiari. Kozi zinazohitajika ni masomo ambayo wanafunzi wote lazima wafanye ili kuhitimu. Kwa mfano, Kiingereza na hisabati ni kozi zinazohitajika.

Baadhi ya masomo ya shule ya upili yana viwango tofauti vya ugumu. Kwa mfano, somo la Kiingereza linaweza kuwa la kawaida, boreshwa au somo la heshima. Hapa kunaya baadhi ya masomo tofauti katika shule ya upili:

- Kiingereza
- Hisabati (Kwa mfano, aljebra au jometri)
- Sayansi (Kwa mfano, bayolojia au kemia)
- Sayansi ya Familia & Mtumiaji
- Jimu/Elimu ya Kimwili
- Sayansi ya Kompyuta
- Teknolojia ya Biashara Inayotekelezwa
- Sayansi ya Jamii
- Sanaa Murua
- Lugha za Kigeni
- Kiingereza kama Lugha ya pili (ESL o ELL)

MADOKEZO MUHIMU

Hifadhi folda ya nyaraka zote za shule. Kila mara watoto watoto wanawapelekea wazazi habari ya shule kwenye mikoba yao.Folda hii inaweza kuweka habari kuhusu, kalenda ya shule, ratiba ya basi, likizo za shule, likizo, na vifaa vingine na matangazo yaliyotumwa kutoka shuleni.

Maelezo ya Ziada

5. Ikiwa mtoto wangu ana matatizo au mahitaji maalum, je, shule itafanya nini ili kusaidia?

Elimu maalum ni programu ya wanafunzi walio na matatizo Fulani shuleni. Wanafunzi hawa wanaweza kuwa na matatizo ya kuona, kusikiza, kuongea, kutembea, kusoma, au kitabia darasani. Shule hutua huduma maalum za elimu kwa wanafunzi ili kuwasaidia kufaulu shuleni. Ikiwa mtoto wako ana mahitaji ya elimu maalum:

- Ulizia kuhusu huduma zinazopatikana katika shule ya mtoto wako.
- Ambia shule aina gani ya msaada maalum ambao mtoto wako anahitaji shuleni.
- Ulizia mkalimani katika mikutano ikiwa huzungumzi Kiingereza.
- Hifadhi nyaraka zote muhimu na barua ambazo mfanyakazi wa shule hupeana au kukutumia.

MADOKEZO MUHIMU

Unaweza kupaka kijitabu kuhusu haki za wanafunzi walemavu kutoka Bodi ya Elimu ya Jimbo la Idaho. Piga simu kwa *SHULE YAKO* na ulizia nakala ya *Mwongozo wa mzazi: Haki za Elimu ya Wanafunzi walio na Ulemavu.*

6. Je, kunazo program maalum ikiwa mtoto wangu ana kipaji au uwezo maalum?

Wanafunzi ambao wana vipaji maalum au uwezo wakati mwingine wanaitwa "Walio na vipawa" au "Walio na talanta". Wanafunzi hawa wakati mwingine wanaweza kuchukua masomo maalum yalio na ugumu zaidi na kazi ya ubunifu.

VIII. JUKUMU LA WAZAZI KATIKA ELIMU NA MASOMO YA WATOTO WAO

Shule zinataka wazazi kuhusishwa katika elimu ya watoto wao. Wazazi wanaweza kuhusishwa katika shule za watoto wao kwa njia nyingi. Wanaweza:

- Kuzungumza na waalimu wakuu na waalimu
- Kuhudhuria shughuli za shule
- Kusaidia kufanya uamuzi kuhusu shule
- Kujitolea shuleni

1. Nitajifunza vipi kuhusu shule ya mtoto wangu? Je, mtoto wangu ni mwanafunzi mzuri?

Shule zina njia tofauti za kuambia wazazi kuhusu programu za shule na maendeleo ya elimu ya watoto wao. Shule nyingi zina:

Nyumba Zilizofunguliwa saa za wazazi kupatana na wazazi wa watoto wao, kuona madarasa yao, na kusikia kuhusu kazi watoto wao wanaifanya.

Kongamano la Mzazi - Mwalimu mikutano kati ya wazazi na waalimu. Mzazi anapatana kisiri na wazazi wa kila mtoto ili kujadili maendeleo ya mtoto au tabia yake darasani. Kwa kawaida waalimu huitisha angalau kongamano moja wakati wa kumalizika kwa mwaka wa shule. Hata hivyo, ikiwa mtoto ana matatizo mengine ya kusoma na ya kitabia, mwalimu atawauliza wazazi kuhudhuria kongamano wakati mwingine wa mwaka. Wazazi pia wanaweza kuitisha kongamano wakati wowote. Wazazi wanaweza kumpigia mwalimu simu au kumwandikia mwalimu maelezo wakimuulizia kongamano. Kongamano za kila mara zinafanyika kabla au baada ya siku ya shule.

Vifaa Vilivyoandikwa vinatumwa nyumbani au kuletwa nyumbani na watoto. Kwa mfano, shule zinaweza kutuma vifaa hivi nyumbani:

- Kalenda za shule kuhusu kazi ya darasani, shughuli za darasani, likizo, au programu za shule
- Majarida yanayozungumzia yale yaliyofanyika madarasani na shuleni
- Usoroveya unaowauliza wazazi hoja zao na matakwa
- Fomu za idhini za wanafunzi kuenda safari za ugani
- Matangazo ya mikutano ya shule, kongamano, mikutano ya heshima, kufunga kwa shule, na matukio mengine
- Wakati mwingine wanahitajika kujibu vifaa vya maandishi. Kwa mfano, lazima utie sahihi kwenye fomu ya kibali kabla watoto wako waweze kwenda katika safari ya ugani.

Kupiga Simu na Mtandao ni njia nyingine ambazo shule huwasiliana na wazazi. Waalimu kila mara hutumia simu kuzungumza na wazazi. Wakati mwingine unaweza kuwa na kongamano la mzazi na mwaalimu kupitia kwenye simu. Baadhi ya shule zia simu za moja kwa moja za kazi ya nyumbani. Wazazi whupiga nambari bainifu ya simu na kuskia ujumbe kuhusu kazi za nyumbani za watoto wao. Shule nyingi pia zina tovuti ya shule na maelezo kuhusu programu za shule, shughuli za darasa, na jinsi ya kumtumia mwalimu barua pepe.

Wazazi wanaweza kupiga simu shuleni kila wakati wanapokuwa na swali na kuzungumza na waalimu au mwalimu mkuu. Ikiwa unataka kutembelea shule ya mtoto wako, piga simu shuleni kwanza ili kuweka miadi. Unaweza kupiga simu shuleni au kutuma maelezo kwa mwaalimu.



2. Nitajua vipi jinsi watoto wangu wanafanya shuleni?

Kadi za Kuripoti: Kadi za ripoti huwaonyesha wazazi jinsi watoto wako wanavyofanya shuleni. Kadi za ripoti huorodhesha somo ambalo mtoto hufanya. Kwa kila somo, kuna gredi. Wazazi hupokea kadi za ripoti za watoto wao mara 4 kila mwaka. Kwa kawaida watoto huleta kadi za ripoti nyumbani. Baadhi ya shule hupeana kadi za ripoti kwa wazazi katika Kongamano la wazazi na Mwalimu. Baadhi ya shule nyingine hutuma kadi za ripoti kwenye barua pepe. Wakati wazazi wanapokea kadi za ripoti, wakati mwingine huhitajika kutia sahihi kwenye kadi ya ripoti au bahasha. Kisha watoto wao wanarudisha kadi ya ripoti shuleni.

Gredi: Shule nyingi hutumia gredi hizi kuwaelezea wazazi jinsi watoto wao wanafanya kwa kila somo:

A kazi nzuri zaidi
B kazi nzuri
C kazi ya wastani
D kazi ya chini ya wastani (kazi mbaya)
F kufeli somo (flunking)

A, B, C, na D ni gredi za kupita. Hata hivyo, wanafunzi wa shule za upili lazima wawe na wastani wa alama ya "C" katika mafunzo makuu ili kuhitimu. Gredi ya F inamaanisha kuwa mtoto hajapita somo. Ikiwa mwanafunzi hafauli katika somo, huenda watahitajika kurudia somo tena au kufanya kazi ya ziada ili kupata gredi ya kupita.

Waalimu wanaamua gredi zipi za kuwapa watoto. Waalimu huangalia kazi ya shule ya watoto, kazi ya nyumbani, na majaribio ili kuwasaidia kuamua gredi za kupeana. Waalimu pia wanatazama na kusikiza watoto shuleni.

Ripoti za Maendeleo: Baadhi ya shule hupeana ripoti za muda mfupi au maendeleo. Wazazi hupokea ripoti hizi katikati ya kadi za ripoti. Katika baadhi ya shule, wazazi wa kila mwanafunzi hupokea ripoti ya maendeleo. Ripoti hizi za maendeleo huonyesha wazazi jinsi watoto wanavyofanya katika kila somo. Katika shule nyingine, wazazi pekee wa wanafunzi walio na matatizo hupokea ripoti ya muda mfupi. Ripoti hizi huonyesha wazazi kuhusu matatizo ambayo watoto wao wanayokumbana nayo katika masomo Fulani.

3. Nitasaidiaje kufanya uamuzi kuhusu shule?

Wazazi wanaweza kuwasaidia watawala wa shule kufanya uamuzi kuhusu programu za shule. Shule zinawaalika wazazi kuhudhuria mikutano ya vikundi tofauti vya wazazi. Wazazi wanaweza kupeana hoja na ushauri kuhusu programu katika shule za watoto wao wakati wanahudhuria mikutando ya kikundi hiki.

- *Wazazi wa wanafunzi wa Kiingereza wa Boise* ni vikundi vya wazazi ambao wanapeana ushauri na hoja kwa shule ili kuimarisha programu maalum kama vile ESL.
- *Kamati/Timu za Kuboresha Shule* huunda mipango ya jinsi ya wafanyakazi wa shule, wazazi, na jumuiya wanaweza kuboresha mafunzo ya mwanafunzi.

- *Mashirika ya Mzazi -Mwalimu* hupanga programu ili kusaidia shule. Kwa mfano, shirika la mzazi – mwalimu linaweza kupanga onyesho la kitabu ili kuuza vitabu. Wanaweza kutumia pesa ambazo wamepata kununua kompyuta za madarasa.

4. Ni shughuli zipi maalum ambazo naweza kuhudhuria katika shule ya watoto?

Shule kila mara hualika wazazi katika shughuli maalum ya shule. Shughuli hizi huwapa waalimu, wazazi, na watoto muda wa kujuana na kila mmoja.

Wakati mwingine wazazi huja shuleni kuwaona watoto wao katika shughuli kama vile:

- Matukio ya riadha ili kuona watoto wao wakicheza michezo kama vile kandanda, mpira wa wavu, au mpira wa vikapu.
- Hucheza na maonyesho ya muziki ili kuona watoto wao wakiigiza, kuimba, aukucheza ala.
- Mikutano kama vile sherehe za kuhitimu au usiku wa heshima ili kuona watoto wao wakipokea heshima au zawadi.
- Wazazi wa Wanafunzi wa Kiingereza wa Boise.

Shule pia hualika familia katika shule ili kujifunja habari mpya. Baadhi ya shughuli hizi ni:

- *Usiku wa Mtaala* ili kuonyesha wazazi kile ambacho watoto wao watajifunza wakati wa mwaka wa shule. Mwalimu pia anaweza kufafanua kile wanafunzi wanapaswa kujifunza ili kupandishwa katika gredi inayofuata au ili kuhitimu.
- *Warsha za Wazazi* ili kuwapa wazazi hoja kuhusu kuwakuza watoto wao. Wazazi wanaweza kujifunzi jinsi ya kuwasaidia watoto wao kuwa na afya na ufanisi. Kwa mfano, warsha inaweza husu jinsi ya kumweka mtoto shuleni na wala sio kuwacha shule. Warsha za wazazi pia zinaweza kuwafunza wazazi jinsi ya kuwasaidia watoto wao kusoma. Kwa mfano, wazazi wanaweza kuhudhuria warsha ili kujifunza jinsi ya kuwasomea watoto wao wachanga vitabu.
- *Miondoko ya Shule* ni mikutano ya wazazi na wanafunzi wapya. Kila mara miondoko inafanyika ya wazazi wa chekechea, mwaka wa kwanza wa shule ya kati au shule ya ngazi ya chini na mwaka wa kwanza katika shule ya upili. Wazazi hupokea habari kuhusu shule mpya ambayo watoto wao watahudhuria. Kwa mfano, wazazi wanaweza kujifunza kuhusu msimbo mpya wa anwani ya shule. Wazazi pia wanaweza kujifunza jinsi ya kusaidia watoto wao kuchagua kozi.

Wakati mwingine shule huwa na shughuli za jamii za wazazi na familia kwenye jumuiya kama vile maonyesho ya kimataifa, Siku ya Kuwashukuru wazazi, na Siku ya kuonyesha Ujasiri. Familia zinakuja shuleni ili kujifurahisha wenyewe. Kwa mfano, wanaweza kuonja vyakula tofauti kutoka nchi nyingi kwenye onyesho la kimataifa.

5. Ni njia zipi ambazo naweza kujitolea katika shule ya watoto wangu?

Wakati mwingine shule zinahitaji msaada wa shughuli za shule. Shule huwauliza wazazi kujitolea kwa shughuli tofauti.

Kwa Shughuli za Darasa na Kusoma unaweza kujitolea:

- kuzungumzia masomo kuhusu kazi yako au nchi yako ya uraia
- kuenda katika safari ya ugani na darasa
- somea darasa au kusikiliza wanafunzi wakisoma

Kwa Programu za Shule unaweza kujitolea:

- kusaidia dansi ya shule
- kuleta vinywaji wakati wa mkutano wa wazazi
- kupanga uchanjishaji wa pesa
- kusaidia kutafsiri
- kusaidia shughuli za Wazazi wa Wanafunzi wa Kiingereza wa Boise

Kuna njia nyingi za wewe kushiriki katika shule. Shule zinahitaji msaada wako, hoja, nakushiriki katika elimu ya watoto wako. Wewe ni kiungo muhimu katika elimu. Unakaribishwa kila wakati shuleni.

6. Nitafanya nini nyumbani ili kusaidia masomo ya watoto wangu?



Wanafunzi walio na ufanisi wanakuja shuleni wakiwa tayari kusoma na kuwa na mazoea thabiti ya kusoma. Kuna njia nyingi ambazo wazazi wanaweza kutumia ili kuwasaidia watoto wao kufanya vizuri shuleni. Unaweza kusaidia hata ikiwa unazungumza Kiingereza kidogo. Sio lazima ujue Kiingereza ili kusaidia. Hapa kuna vitu muhimu ambavyo unahitaji kujua ili kumsaidia mtoto wako masomoni:

Nguoa za Hali ya anga: Hakikisha nguo za mtoto wako ziko sawa kulingana na hali ya anga huko nje. Kwa mfano, ikiwa kuna baridi nje, wanafaaa kuvaa nguo za joto kama vile koti, kofia na glovu.

Sare za Shule na Msimbo wa Mawazi: Katika baadhi ya shule wanafunzi lazima wavae sare wakienda shuleni. Kwa mfano, sare inaweza kuwa shati nyeupe na kaptula au sketi za samawati. Shule nyingine hazina sare ya shule, lakini wana misimbo ya mavazi. Msimbo wa mavazi ni kanuni maalum kuhusu mavazi ambayo watoto wanaweza kuvaa wakienda shuleni. Kwa mfano, katika baadhi ya shule wavulana haweawezi kuvalia kofia na wasichana hawaruhusiwi kuvalia shati tao nusu. Ikiwa waoto wako hawajavalia ipasavyo shuleni, baadhi ya shule zitawarudisha nyumbani.

Vifaa vya Shule: Watoto wanahitaji kuleta vifaa darasani. Vifa vya shule ni karatasi, penseli, kalamu, na vifutio. Wakati mwingine watoto wanahitaji vifaa vingine kama vile rula, makasi, au gundi. Kwa kawaida waalimu watawapatia wanafunzi orodha ya vya shule ambavyo wanahitaji. Ikiwa huwezi kununua vifaa, mwambie mwalimu.

Kuzungumza kuhusu Kazi ya shule: Wazazi wanapaswa kuwauliza watoto wao kila siku, "Shule ilikuwa aje leo?" "Una kazi yoyote ya nyumbani usiku wa leo?" Shule zinakuhitaji kujadili kazi ya shule na watoto wako. Unaweza kuwauliza watoto wako kile wanachojifunza katika madarasa yao. Pia unaweza kuwauliza watoto wako kuleta nyumbani na kukuonyesha makaratasi yao yaliyo nwekwa gredi.

Kusaidia kufanya Kazi ya nyumbani: Kazi ya nyumbani ni kazi ambayo waalimu wanawapatia wanafunzi ili kufanyia nyumbani.

MADOKEZO MUHIMU

Shule zinaweza kuorodhesha nafasi za watu wa kujitolea kwenye jarida la shule, kwenye ukurasa wa wavuti wa shule, au kwenye matangazo maalum yanayo tumwa nyumbani kutoka shuleni.

Kuna aina tofauti za kazi za zoezi la nyumbani. Watoto wanaweza:

- kukamilisha kazi walizozianza shuleni
- Kufanya kazi ambayo ni ya mazoezi au kuhakiki kile walichojifunza shuleni (kama vile kusoma au hisabati)
- Kufanya miradi maalum, kama vile ripoti za vitabu, majaribio ya sayansi au kuchora ramani
- Kusomea swali au jaribio

Waalimu wanaamua kiwango cha kazi ya nyumbani ya kupeana kila usiku. Sio waalimu wote hupeana kiwango sawa cha kazi ya nyumbani. Watoto wakubwa kwa

kawaida huwa na kazi nyingi ya nyumbani kuliko watoto wachanga. Hapa kuna baadhi ya vitu unavyohitajika kufanya ili kuwasaidia watoto wako na kazi ya nyumbani:

Muda wa Kazi ya nyumbani: Watoto wana shughuli nyingi za kila siku kama vile kazi ndogondogo, miadi, muda wa kucheza, programu za baada ya shule, na kazi ya nyumbani. Ni bora ikiwa kazi ya nyumbani itafanywa kwa wakati mmoja kila alasiri au jioni, lakini sio usiku kabisa. Wakati wa saa ya kazi ya nyumbani, unapaswa kuzima runinga na michezo ya video/kompyu. Watoto wanahitaji mahali patulivu ili kufanya kazi yao ya nyumbani.

Kuangalia kazi ya nyumbani: Unaweza kuangalia kazi ya nyumbani kuona ikiwa ni safi na imekamilika. Watoto wako wanaweza kukuelezea kazi yao ya nyumbani. Wakati mwingine watoto huona makosa wanapokueleza kazi yao ya nyumbani.

Matatizo ya kazi ya nyumbani: Wakati mwingine watoto hawawezi kukamilisha kazi yao ya nyumbani kwa sababu hawaielewi. Ikiwa wazazi wanaelewa kazi ya nyumbani wanaweza kuwasaidia watoto wao, lakini wazazi hawapaswi kufawafanyia watoto wao kazi ya nyumbani.

Wazazi wengi hujihisi kuwa hawawezi kuwasaidia watoto wao na kazi ya nyumbani. Wakati mwingine wazazi hawaelewi Kiingereza zaidi au hawaelewi somo. Ikiwa wazazi hawawezi msaidia mtoto na matatizo ya kazi ya nyumbani, wanapaswa kuandika maelezo au kumpigia simu mwalimu wa mtoto. Wazazi wanaweza kumwambia mwalimu mtoto wao alikuwa na tatizo la kukamilisha kazi. Wakati mwingine watoto wanaweza kupata msaada wa ziada wa kazi yao ya nyumbani shuleni kabla ya shule kuanza, baada ya shule, au wakati wa mapumziko.

Wakati mwingine watoto hawataki kufanya kazi yao ya nyumbani. Wanaweza kupata muda wa kutazama runinga au kucheza, lakini hawana muda wa kufanya kazi ya nyumbani. Kila mara waalimu watapiga simu au kuwaandikia maelezo wazazi ikiwa mtoto hafanyi kazi ya nyumbani. Waalimu na wazazi lazima waamue kile kitakachjofanyika kwa watoto ambao hawafanyi kazi ya nyumbani. Waalimu kwa kawaida huwapa wanafunzi gredi ya chini.

Maktaba: Kwa kazi nyingine za nyumbani watoto huenda wakahitaji vifaa kutoka kwenya maktaba ya umma. Vifaa vyote vya maktaba vinaweza kutumiwa kwenye maktaba. Ikiwa mtoto wako anataka kwenda na vifaa nyumbani au kutumia kompyuta za maktaba, lazima uwe na kadi ya maktaba.

Unaweza kupata kadi ya maktaba kwenye maktaba. Chukua bili au waraka mwingine ambao unaonyesha thibitisho la anwani yako.

Kusoma na Kuongea Pamoja: Watoto ambao wanasoma nyumbani hufanya vizuri shuleni. Ni hoja nzuri kutenga wakati wa familia kusoma nyumbani kwako. Wakati wa kusoma unaweza kuwasomea watoto wako, watoto wako wanaweza kukusomea, au kila mmoja anaweza kujisomea wakati wa kusoma. Ni muhimu watoto wako kukuona ukisoma katika Kiingereza au kwenye lugha yako ya uraia.

Ikiwa kusoma kunakuwa vigumu kwako, wasimulie watoto wako hadidhi. Unaweza kuwasimulia hadithi kuhusu familia yako wakati ulikuwa mdogo na kuhusu watoto wako walipokuwa wachanga. Watoto wako pia wanaweza kusimulia hadithi. Unaweza kusimulia hadithi kwa lugha ya kiingereza au lugha yako ya uraia.

Shughuli za Kusoma za Familia na Vituo vya Rasilimali ya Familia: Shule nyingi na mashirika ya jumuiya hutoa programu za kusoma za familia jioni na wikendi. Wazazi na watoto huhudhuria shughuli hizi pamoja. Familai yako inaweza kujifunza kuhusu masomo kama vile hisabati, sayansi, kusoma, na kompyuta. Kwa kawaida utapokea vifaa vya kupeleka nyumbani kwa usamoja zaidi.

Baadhi ya shule zina vituo vya rasilimali vya familia. Vituo hivi vina vifaa ambavyo wazazi wanaweza kuazima na kupeleka nyumbani. Baadhi ya vifaa vinahusu maendeleo ya mtoto, mulo, usalama, afya, shule, na shughuli za masomo. Kwa kawaida kuna vitabu, michezo, video, vinasa rekodi, na rekodi za sauti.

7. Nitafanya nini ili kusaidia watoto wangu kupanga maisha yao baada ya shule ya upili?

Wazazi wanafaa kuwajua wafanyakazi wa shule ambao wanaweza kusaidia na mipango ya siku za usoni ya watoto wako. Mshauri wa kuongoza shule ya upili au mshauri wa kazi anaweza kusaidia familia kufanya uamuzi kuhusu kile ambacho wanafunzi wanapaswa kufanya baada ya shule ya upili. Wakati mtoto wako anaanza shule ya upili, anza kuzungumza kuhusu mipango ya siku za usoni. Ni bora kufanya uamuzi kabla ya mwaka wa mwisho katika shule ya upili. Ikiwa watoto wanaamua kama wamechelewa kwenda katika chuo cha elimu ya juu, huenda wasipate kozi zote ambazo wanahitaji. Wanafunzi wanahitaji kufanya kozi nyingine katika shule ya upili ili kuwaandaa kwa chuo cha elimu ya juu. Wanafunzi pia wanahitaji majaribio katika shule ya upili ili kuomba nafasi katika chuo cha elimu ya juu.

MADOKEZO MUHIMU

Wasiliana na shule ya mtoto wako ili kujua ikiwa wana kituo cha usaidizi cha familia au shughuli za kujifunza za familia.

IX. ELIMU YA WATU WAZIMA

1. Nitaenda wapi kujifunza Kiingereza au kuhudhuria masomo mengine?

Kuna nafasi nyingi za kusoma za watu wazima. Mafunzo mengi ni ya bila malipo, lakini mengine yanalipisha ada ya masomo. Masomo yanafanyika wakati wa mchana na jioni. Masomo ya watu wazima kila mara yanafanyika katika vyuo vya elimu ya juu vya jumuiya, shule, maktaba, na vituo vya jumuiya.

Baadhi ya masomo ya elimu ya watu wazima ni:

- **Kiingereza kama Lugha ya Pili (ESL)** – ujuzi wa kawaida wa lugha ya Kiingereza.

- **GED na Ujuzi wa Kawaida** – usomaji wa kawaida na ujuzi wa hisabati, na kuandaa jaribio la GED (kukamisha shule ya upili).

Kunazo pia programu za academia katika vyuo vya elimu ya juu na vyuo vikuu kama Jimbo la Boise. Programu za academia huwaandaa watu wazima kwa masomo ya chuo cha elimu ya juu na kulipisha ada ya masomo.



Kwa maelezo ya ziada angalia mtandao katika Elimu ya Kawaida ya Watu wazima katika Idaho - For additional information look on the internet at Idaho Adult Basic Education – Taasisi ya Taifa ya Kusoma na Kuandika: http://www.nwlincs.org/idalincs/

MADOKEZO MUHIMU

Unaweza kupata maelezo kuhusu elimu ya masomo ya watu wazima kutoka:

- **shule ya mtoto wako**
- **Maabara ya Kusoma**
- **maktaba yako ya umma**
- **Chuo kikuu cha Jimbo la Boise**
- **Mashirika ya kidini au kabila**
- **Chuo cha elimu ya juu cha Idaho Magharibi**

SHULE YA WILAYA YA BOISE

KARIBU KATIKA SHULE ZA BOISE
KUTOKA KWA MSIMAMIAJI WETU

Dkt. Don Coberly

Shule Huru za Wilaya ya Mji wa Boise

Kwa Wazazi na Walezi:

Karibu katika Shule ya Wilaya ya Boise! Tunafurahia kuwa na wewe pamoja na wanafunzi wako kama sehemu ya jamii yetu. Tunatathmini kila mwanafunzi na kufanya kazi ili kuboresha nguvu za watu binafsi na kuimarisha mahali ma udhaifu. Boise inazo programu nyingi ambazo zinapatikana za kukuza na kuongeza kasi ya uzoefu wa elimu ya wanafunzi wako wanapojiandaa kwa chuo cha elimu ya juu na kazi.Waelimishaji waliohitimu zaidi wanaongoza programu hizi.

Tumefurahia kuwa pamoja na familia yako kama mmoja wa Wilaya yetu. Ikiwa una maswali yoyote au unataka maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na shule yako ya karibu (wanaweza kukalimani ikiwa unahitajika). Ushiriki wako katika Shule za boise ni muhimu kwa ufanisi wa wanafunzi wako na Wilaya yetu.

Mwaminifu,

Don Coberly

Dkt. Don Coberly
Msimamiaji

Kuelimisha Leo kwa ajili ya Kuboresha Kesho…

1. Nitamwandikisha vipi mtoto wangu?

Ikiwa kuna lugha nyine nyumbani kwako, lazima umpigie simu Diane, *Mtaalam wa kusajili* wa Boise kwanza. Mtaalam anaweza kufikiwa kwa 472-3097 kati ya 7:00 asubuhi na 2:30 jioni. Watakusaidia na kazi yote ya makaratasi na kukutambulisha shuleni, kwa mwalimu mkuu na mwalimu.

2. Ni shule gani ambayo mtoto wangu atajiunga nayo?

Mtoto katika **kiwango cha msingi** (gredi za K – 6) anapelekwa katika shule ya ELL ikiwa wanahitaji usaidizi wa lugha. Wanafunzi kila mara wanawekwa pamoja na watoto walio na umri wa miaka sawa.

Mwanafunzi kati **kiwango cha sekondari** (gredi za 7 – 12) wataenda kwa programu ya Borah au Hillside Bridge **au** katika shule ya ngazi ya chini ya karibu (gredi za 7 – 9) au shule ya upili (gredi za 10 – 12).



3. Ni programu zipi ambazo Boise inazo kwa wanafunzi wa shule ya ngazi ya chini na ya upili?

Programu ya **Kuunganisha** (Wanafunzi Marekani chini ya miaka 2) waalimu wa ELL hufundisha Kiingereza, Hisabati, Sayansi, na masomo mengine.

Shule ya Karibu ya Ngazi ya chini/ upili (Wanafunzi Wanaozungumza Kiingereza cha Kati/Kilichoboreshwa) Waalimu maalum hufundisha masomo mengi yakiwemo Kiingereza, hisabati, Sayansi na Historia. Waalimu husaidia maagizo ya darasani na kazi ya nyumbani.

4. Mtoto wangu atafika vipi shuleni?

Diane Goicoechea-Price atasaidia kuratibisha usarifi wa basi kwa wanafunzi wa ELL. Piga simu 472-3097.

Inachukua siku tano (5) za kufanya kazi kabla ya basi kumchukua mtoto wako. Mtoto wako hatapata basi ikiwa unaishi maili 1 ½ (Kilomita 2.4) au chini kutoka shuleni.

Maelezo ya Ziada

5. Nitalipia nini shuleni?

- Wanafunzi wanaweza kununua kiamsha kinywa au chakula cha mchana shuleni. Wanaweza kupata chakula cha mchana cha bila malipo au kilichopunguzwa gharama. (tazama bei katika boiseschools.org)
- Wanafunzi wanaofanya P.E katika shule ya ngazi ya chini au ya upili lazima walipe $5 ya dawati.
- Kuna ada ya sanaa, fotoaji picha na masomo mengine ya aina hii.

Menyu za Msingi

Kiamsha kiny

Chaguo

Aina tofauti ya nafaka
Tosti
Maziwa
Maji ya Machungwa

Kiamsha kinywa chote cha bila malipo ni sharubati na maziwa.

Chakula cha

Chaguo

Tunapeana aina 3 ya machaguo yote kila siku, pamoja na aina tofauti ya maziwa. Watoto wataweza kuchagua aina tofauti ya matunda, mboga na mikate kutoka kwa Mwambaa wetu wa Chaguo za Kiafya ili kuambatana na chakula kingine.

Watoto wa chekechea wanaweza kula kiamsha kinywa na/au chakula cha mchana shuleni ama baada au kabla ya masomo.

Menyu ya Sekondari

Kiamsha k

Chaguo

Rolu ya Mdalasini
Bagel
Kiamsha kinywa cha Burrito
Mgando
Nafaka Mbali mbali Baridi

Kiamsha kinywa chote kinajumlisha sharubati chaguo lako la maziwa kidogo au mengi.
Baadhi ya shule hupeana kiamsha kinywa asubuhi na mapema. Kiamsha kinywa kinapatikana.

Chakula c

Machaguo Murua

Yanaweza kujumlisha:
Hamburger
Burrito
Aina ya Pizza
Tacos
Nageti za Kuku
Sandiwichi Moto & Baridi

Mwambaa wa Kujihudumia Mwenyewe

Inaweza kujumlisha:
Pasta Alfredo
Kuku ya Nchi
Taco Loco
Asian Noodles
Kuku Tamu & Chacha

Uteuzi Mkuu

Jina la Bidhaa Pizza
Sandiwichi za Deli Zilitengenezwa ili Kuweka Oda

Pokea kuki iliyotengenezewa nyumbani wakati unatumia kadi yako ya mlo!
Chakula chote cha mchana kinaandaliwa pamoja na sharubati, mboga & maziwa.
Mboga & vyakula vya mafuta kiasi vinapatikana kila siku, tafadhali uliza.

6. Je, mtoto wangu anaweza kuchelewa au kukosa kwenda shuleni?

Tadi (kuchelewa shuleni): Mwanafunzi anachelewa ikiwa hayuko kwenye darasa lililopewa kazi wakati kengele inapolia. Ikiwa mwanafunzi amechelewa kwa zaidi ya dakika ishirini (20) katika darasa, atazingatiwa kukosekana. Wanafunzi wanaweza kuchelewa (tadi) mara sita kwa kila darasa kila kipindi. Kuchelewa kwa mara ya sita (6) mwanafunzi wako atahitajika kuhudhuria shule Jumamosi. Mwanafunzi lazima arudie darasa ikiwa atakosa kwa mara sita.

Kukosa kifika shuleni kwa Radhi: Mwanafunzi anaweka kukosa hadi siku tisa (9) kila kipindi kwa kila somo. Mzazi au Mlezi lazima awasiliane na shule kati ya saa 48 za kuomba (fafanua) kukosa. Ikiwa kukosa kufika kunakubaliwa na mzazi amewasiliana na shule, mwanafunzi anaweza kufanya kazi yoyote ya nyumbani au mazoezi. Ikiwa mwanafunzi anakosa zaidi ya siku tisa (9) lazima wakamilishe "Rufaa" (ombi lililoandikwa ili kupokea alama ya somo).

Kukosa kufika bila Radhi/trunzi: Ikiwa mwanafunzi amekosa kufika, au anatoka shuleni, bila ya mzazi kuwasiliana na afisi hana radhi au ni tranti. Ikiwa atakosa kufika kwa zaidi ya siku tisa (9) kwa kila kipindi, anaweza kupoteza alama. Hataruhusiwa kukamilisha mazoezi yoyote aliyoyakosa wakati huo. Inaweza kuathiri mchakato wa rufaa. Wanafunzi huenda wakasimamishwa au kufukuzwa.

7. Je, mwanafunzi wangu anaweza kuondoka shuleni wakati wa mchana?

Mzazi anaweza kuwasiliana na shule ili kupeana kibali cha mtoto wao kuondoka shuleni wakati wa chana. Mwanafunzi lazima atie sahihi afisini kabla ya kuondoka wakati wa mchana. Kuondoka bila kibali na bila ya kwenda afisini kutatokana na marejeleo ya Nidhamu. Wanafunzi hawapaswi kuwa katika eneo la uegezaji wakati wa chakula cha mchana au mapumziko.

8. Ni nini kinachokataliwa shuleni?

Bipa, peja, simu za rununu, kalamu za leza, njiti, bunduki za skuati, minyororo zinazoning'inia kutoka kiunoni zimekataliwa.

Mavazi ya kufunika kichwa (ila tu kwa sababu za kidini) hayaruhusiwi shuleni.

Dawa, pombe na tobako (sigara) pia zinakataliwa. Wanafunzi wanaweza kusimamishwa kutoka shuleni, au hata kufukuzwa. Mwanafunzi atapelekwa kwa polisi

Rejeleo lolote au msaada wa wezi unakataliwa. Hakuna mavazi ya alama za uchochezi yatavaliwa au kutekelezwa ambayo yanachukiza dini nyingine au kikundi cha kitamaduni. Wanafunzi wanaweza kusimamishwa kutoka shuleni, au hata kufukuzwa.

Lugha ya matusi au ya kutokumcha haikubaliwi. Vitisho vilivyoandikwa au vya maneno havitavumiliwa. Kupigana hakuruhusiwi. Wanafunzi wanaweza kufukuzwa kutoka shule ya wilaya kwa kutoa vitisho.Mwanafunzi anaweza kupelekwa kwa polisi.

9. Ni nini kitafanyika kwa mwanafunzi ambaye huleta silaha shuleni?

Mwanafunzi anayemiliki silaha (bastola, kisu cha kibindo, mesi, n.k.) atafukuzwa kutoka shule ya wilaya. Mwanafunzi atapelekwa kwa polisi.

10. Naweza kupata wapi maelezo ya ziada kuhusu Shule ya Wilaya ya Boise?

Unaweza kupata maelezo ya ziada kuhusu shule ya wilaya katika tovuti yetu: http://www.boiseschools.org/ au kwa kupiga simu 854-4000.



11. Nitapata wapi maelezo kuhusu Programu za Kiingereza kwa Mwanafunzi?

Kwa maelezo ya ziada ya ELL tembelea tovuti yetu katika:
http://www.boiseschools.org/ell/index.html

Unaweza pia kuwasiliana na yeyote kati ya watu wafuatao:

Diane Goicoechea-Price
Mtaalam wa kusajili
472-3097
diane.goicoecheaprice@boiseschools.org

Jolene Lincoln
Mshauri wa Programu za Shirikisho
854-4379
jolene.lincoln@boiseschools.org

Stacey Roth
Mwalimu Mshauri wa ELL
854-4379
stacey.roth@boieschools.org

Molly Jo de Fuentealba
Mshauri wa Programu za Shirikisho
854-4379
molly.fuentealba@boiseschools.org

Cindy Daly
Mshauri wa Programu za Shirikisho
472-3593
cindy.daly@boiseschools.org

Dr. Ann Farris
Mtawala wa Programu za Shirikisho
854-4133
ann.farris@boiseschools.org

Maelezo ya Ziada